* 0000800000001 * DFD

CAMBRIDGE
International Education

# Cambridge IGCSE™

| | | | |
|---|---|---|---|
| CANDIDATE NAME | | | |
| CENTRE NUMBER | | CANDIDATE NUMBER | |

**SWAHILI** **0262/01**

Paper 1 Reading and Writing **May/June 2026**

**2 hours**

You must answer on the question paper.

No additional materials are needed.

**INSTRUCTIONS**
- Answer **all** questions.
- Use a black or dark blue pen.
- Write your name, centre number and candidate number in the boxes at the top of the page.
- Write your answer to each question in the space provided.
- Do **not** use an erasable pen. Do **not** use correction fluid or tape.
- Do **not** write on any bar codes.
- Dictionaries are **not** allowed.

**INFORMATION**
- The total mark for this paper is 60.
- The number of marks for each question or part question is shown in brackets [ ].

This document has **16** pages. Any blank pages are indicated.

DC (WW) 364783/3
© Cambridge University Press & Assessment 2026

**[Turn over**

https://xtremepape.rs/

## Zoezi 1

Soma kifungu kifuatacho kuhusu fisi maji halafu jibu maswali yanayofuata.

Likizo iliyopita niliogelea na fisi maji katika mapango yaliyo kusini mwa kisiwa cha Unguja. Fisi maji ni aina ya mamalia wanaoishi ardhini na pia majini. Jina lao linamaanisha wao ni fisi wanaoishi majini, ingawa mimi sikuhisi kama walifanana na fisi. Ninadhani wanafanana na nguchiro. Ingawa huonekana weusi kwa mbali, rangi yao halisi ni kijivu iliyochanganyika na kahawia. Miili yao ina manyoya yanayoteleza ambayo ni malaini.

Mwanzoni niliogopa kuingia majini na kuogelea na fisi maji kwa sababu waongozaji waliofanya kazi hapo walituambia kwamba wangeweza kung'ata. Kwa vile mimi nilikuwa na hamu ya kuwalisha, walituambia kwamba, ingebidi kunyanyua chakula kwa juu na kukining'iniza ili fisi maji wakidake. Walisema kama mtu atawapa chakula kwa kukiweka juu ya kiganja, basi wangeweza kumng'ata kiganja. Fisi maji hula samaki wadogo kama dagaa. Wanapokuwa katika mazingira yao halisi wao hula wadudu pia.

Baada ya muda, niliona watoto wadogo wakiogelea na fisi maji ndipo nilipopata moyo kuingia majini na kuogelea nao. Kamwe sitaisahau siku hiyo. Tuliambiwa kwamba, kwa kawaida fisi maji hutumia muda wao majini na nchi kavu ingawa wanapotaka kujifungua huenda nchi kavu na hutengeneza kiota kwa kutumia vijiti na majani makavu. Nilisoma mahali kwamba fisi maji hutumia vifaa kama mawe katika shughuli zao. Pia, fisi maji hukaa katika viota vyao na hunyonyesha vitoto vyao humo ndani na huwalisha mpaka wanapokuwa wakubwa.

Katika jadi yao, watu wa Unguja hawali fisi maji kabisa. Pia, niliambiwa kuwa kuna sheria inayokataza wananchi kula fisi maji. Tena, kama watu wakikamatwa wanakula basi wanaweza kufungwa. Mimi ninaamini kwamba hatua zinazochukuliwa na serikali kuhifadhi wanyama ni muhimu sana, ingawa jambo hili ni kero kwa wengi wanaoishi vijijini.

Swali nililojiuliza hasa ni kama fisi maji wanaweza kupumua ndani ya maji. Niliwaza kwamba kama wangaliweza, basi wangaliweza kujificha majini, hasa ndani ya majabali, ili kuepuka wawindaji. Lakini nilifahamishwa kuwa, ingawa fisi maji hupenda kuwa pembezoni mwa maji, wao hawawezi kupumua majini. Wanalazimika kuziba pua na kuogelea juu ya maji ili mapafu yao yapumue.

Unapowatazama fisi maji, utaweza kuwatambua na kuwatofautisha wale wa kike na wa kiume. Tofauti kubwa si ukubwa au udogo wa fisi maji, bali ni uwepo wa titi moja au mawili kwa fisi maji wa kike. Hata hivyo, fisi maji wote hupenda sana kucheza kati yao, ingawa nilitegemea kwamba watoto tu ndio wangependa kucheza.

Kwa kweli nilifurahia sana kuogelea na fisi maji ingawa safari nyingine ninataka kuogelea na pomboo!



DO NOT WRITE IN THIS MARGIN

https://xtremepape.rs/

1 Msemaji anawafananisha fisi maji na mnyama gani?

........................................................................................................................................ [1]

2 Fisi maji wana rangi gani?

........................................................................................................................................ [1]

3 Ili using’atwe, inabidi kumlisha vipi fisi maji?

........................................................................................................................................ [1]

4 Fisi maji hujenga nini nchi kavu?

........................................................................................................................................ [1]

5 Kwa nini watu wa Unguja hawali fisi maji?

..............................................................................................................................................

........................................................................................................................................ [2]

6 Nini maoni ya wanavijiji kuhusu uhifadhi wa fisi maji?

........................................................................................................................................ [1]

7 Tunajuaje kwamba fisi maji wanafurahi wanapokuwa pamoja?

........................................................................................................................................ [1]

[Jumla: 8]

DO NOT WRITE IN THIS MARGIN

© Cambridge University Press & Assessment 2026

https://xtremepape.rs/

## Zoezi 2

Wanafunzi wanne wanaelezea kuhusu kusoma vitabu.

**A Ali**

Kabla ya kulala ni lazima nisome angalau kurasa tano au zaidi, kwa hivyo nina rafu la vitabu kando ya kitanda changu kwani ni rahisi kwangu kuchagua kitabu cha kusoma. Ndugu zangu pia huviazima. Rafu langu lina vitabu nivipendavyo zaidi kuliko vyote. Vitabu hivyo ni vya fasihi, hasa riwaya. Kusoma vitabu hupeleka fikra zangu sehemu tofauti na kunifanya nihisi kama ninawafahamu watu wenye maisha tofauti na yangu. Ninahisi kusoma huniliwaza, hasa pale ninapokuwa na wasiwasi kuhusu mambo tofauti. Mapenzi yangu ya vitabu yamenisaidia shuleni kwani nimeweza kujadiliana na walimu na pia kutoa mawazo yangu kuhusu waandishi wengi. Ninapendelea zaidi waandishi wa Kiafrika ambao hawaishi barani humu. Kwa mawazo yangu waandishi hao wana uwezo wa kuchambua matukio vizuri zaidi kwani wapo mbali. Sijawahi kusoma vitabu vya waandishi wanaoishi nchini kwangu.

**B Bahati**

Nilipokuwa nikifanya utafiti wa kazi niliyopewa na mwalimu shuleni, niligundua kwamba mjomba wangu alikuwa mwandishi maarufu sana Afrika Mashariki. Ameandika riwaya na mashairi mengi ambayo yanasomwa na watu duniani. Nilipoona hivyo, nikawa na ndoto ya kuwa mwandishi kwa hivyo, nikaamua kuanza kujaribu kubuni hadithi na pia mashairi. Nilianza kwa kuandika hadithi fupi ambazo zilikuwa na ushairi kwa wasomaji. Mwaka jana hadithi zangu zilipigwa chapa na nilialikwa kuzisoma katika warsha iliyofanywa maktabani kwetu. Niligundua kwamba kusoma hadithi zangu kulinisisimua na kunipa ujasiri mkubwa wa kutaka kuendelea kuandika na hata kupata pesa za kujikimu. Ningefurahi kama shule yetu ingalikuwa na masomo ya uandishi, au kama wangaliwaalika waandishi wa Kiafrika waliotuzunguka hapa kwetu ili waje kusoma kazi zao na kutupa ari ya kuwasoma. Ninawapenda sana waandishi hao.

**C Charlie**

Nyumba yetu imejaa marafu ya vitabu vya kila aina, kwani sisi tunamiliki vitabu vingi vya kihistoria. Kwa kweli vitabu ni urembo nyumbani, ndio sababu familia yangu inavinunua na hatuviazimi kutoka maktabani. Kwa hivyo, vitabu vyetu haviwezi kuharibika kwani hakuna mtu anayevisoma. Ni mama yangu pekee anayevigusa anapovipangusa vumbi linalojaa vitabuni. Nililazimika kuanza kusoma vitabu wiki iliyopita nilipoanza shule ya upili kwani walimu hutulazimisha kusoma. Ninadhani kama tungepewa vitabu vya wasifu, kwa mfano wasifu wa rais wa nchi yangu, labda ningependa kusoma. Hasa kwa sababu yeye alikuwa maskini na sasa amekuwa mtu muhimu sana duniani. Nilipokuwa mtoto mama yangu hakuwa na muda wa kunisomea vitabu, alimwambia kaka yangu anisomee hadithi. Kwa vile kaka yangu alichukia kufanya hivyo, basi alisoma haraka haraka ili amalize halafu aende kufanya shughuli nyingine. Ninadhani ni yeye aliyenihamasisha kutovutiwa na vitabu na kuona kama kusoma ni kazi inayochosha.

**D Doto**

Rafu lililo chumbani kwangu limejaa mapambo na vipodozi. Vitabu vyangu vyote vipo ndani ya mfuko wangu wa shule ambao mimi huuweka chini ya kitanda changu. Nikiuwacha mfuko wangu sehemu nyingine yoyote, mdogo wangu hupenda kuufungua na kutoa kila kitu halafu kuvitupa ovyo. Kwa maana hiyo mimi hupoteza vifaa vyangu vya shule halafu walimu hukasirika. Mara ya kwanza mimi kuona rafu la vitabu ilikuwa katika maktaba ya shule yetu. Nilianza kuazima vitabu papo hapo na hadi sasa mimi husoma vitabu kutoka maktabani tu. Ni muhimu kuvirudisha baada ya kuvisoma ili watu wengine wavifaidi. Pia, unapochelewa kuvirudisha inabidi kulipa faini. Nitakapomaliza shule na kuanza kazi, nitakuwa na uwezo wa kujinunulia vitabu na kuvipamba katika rafu nyumbani kwangu. Ingawa sina mazoea ya kuandika, nina mpango wa kufanya hivyo siku zijazo kwa starehe yangu na si kama ajira. Hadhira yangu itakuwa watu wa nchi yangu na si watu wa mbali ambao hawaelewi uhalisia wetu.

© Cambridge University Press & Assessment 2026 

DO NOT WRITE IN THIS MARGIN

https://xtremepape.rs/

Soma taarifa (**8–16**) zifuatazo. Weka alama ya tiki (✓) kwenye kisanduku kuonyesha aya (**A–D**) inayohusiana na kila taarifa. Kuna mfano mmoja hapa chini.

**Mfano**

Nani …

husoma kabla ya kulala

**A** ☑ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐

**8** ana rafu la vitabu vyake mwenyewe

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

**9** huhifadhi vitabu mbali na nduguye ili visiharibiwe

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

**10** anaona vitabu kama ajira

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

**11** anaamini ni bora mwandishi kuwa mbali na hadhira yake

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

**12** ana ndoto inayohusu umilikaji wa vitabu

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

**13** anaamini kusoma vitabu kumeathiri fikra zake

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

**14** hana mazoea ya kusoma mwenyewe

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

DO NOT WRITE IN THIS MARGIN



https://xtremepape.rs/

**15** amehamasishwa kuandika na mwanafamilia

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

**16** anazingatia mchakato maalumu wa kusoma vitabu na kutolipa

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

[Jumla: 9]

DO NOT WRITE IN THIS MARGIN



https://xtremepape.rs/

Turn over

DO NOT WRITE IN THIS MARGIN
DO NOT WRITE IN THIS MARGIN
DO NOT WRITE IN THIS MARGIN
DO NOT WRITE IN THIS MARGIN
DO NOT WRITE IN THIS MARGIN



https://xtremepape.rs/

## Zoezi 3

Soma makala yafuatayo kuhusu kutotumia magari mijini.

Siku ya Kutotumia Magari Duniani huadhimishwa kila mwaka tarehe 22 Septemba. Ulimwenguni kote, siku za kutotumia gari huwahimiza watu kuacha magari yao na kutumia usafiri usio wa magari, kama vile kuendesha baisikeli au kutembea. Kwa nchi zenye theluji, watu huweza kuteleza kwenye theluji pia.

Nchi za Kiafrika kama vile Uganda, Ethiopia na Rwanda zimechagua siku maalumu za kila mwezi ambapo magari hayaruhusiwi barabarani. Serikali za nchi hizi zimeamua kufanya hivi ili kupambana na uchafuzi wa hewa, ingawa wafanya biashara wachache wana wasiwasi kwamba watu hawataweza kufika kazini. Serikali hizo zimewashauri watu kutumia fursa hiyo kwa kufanya mazoezi ya pamoja kama vile kucheza mpira wa miguu barabarani au kucheza muziki mitaani. Hii ni tofauti na miji ya Ulaya iliyoendelea kama Oslo, ambapo sehemu maalumu zimetengwa na magari hayaruhusiwi kuendeshwa kamwe. Suluhisho moja zuri ambalo lingefaidisha miji ya Kiafrika inayochagua siku maalumu ya kutoendesha, ni kutafuta teknolojia mpya za usafiri kama baisikeli za umeme ambazo watu wangeweza kuazima na kutumia bila ya kuharibu mazingira. Hii ingeondoa tatizo la kufunga maeneo.

Ingawa kuboresha miundo mbinu ya usafiri barani Afrika kutahitaji mabilioni ya pesa, miji mingi imeshaanza kuchukua hatua za kupunguza matumizi ya magari. Kwa mfano, nchini Uganda, mkakati wa kuwa na siku moja kila mwezi ambapo magari hayaruhusiwi mijini ili kupunguza uchafuzi wa mazingira umeanzishwa. Kauli mbiu ya mpango huo ni “Mimi ndiye suluhisho la uchafuzi wa mazingira.” Hata hivyo, mkakati huu umeweza kufanyika katika miji ya Kampala na Jinja tu, ambayo ni miji mikubwa. Kwa siku hiyo, foleni za magari huwa chache hasa ikilinganishwa na siku nyingine za mwezi ambapo msongamano wa magari huwa mkubwa na huonekana kama jambo la kawaida.

Nchini Ethiopia, siku ya kutotumia magari hupendwa sana. Mamia ya raia huamka alfajiri na kukimbia au kuendesha baisikeli katikati ya mji mkuu. Watu huamka saa kumi alfajiri ili kukimbia. Wanafurahia kutokuwa na wasiwasi wa kugongwa na gari au kupigiwa honi. Miaka inavyoenda, tunaweza kuona ongezeko kubwa la watu wanaojiunga na siku za kutotumia magari ingawa kuna sehemu ya jamii ambayo haiwezi kujiunga na shughuli hizi, kama vikundi vya wazee na walemavu ambao wanategemea magari kurahisisha maisha yao ya kila siku.

Bila shaka kuna watu wengine wanaohisi kwamba, ingawa hawana upungufu wowote, wanahitaji magari ili kubeba bidhaa nzito wanazouza au walizonunua na wanataka uhuru wa kutembelea sehemu tofauti kwa gari.

Nchini Rwanda, zaidi ya kuwepo kwa sherehe ya kila mwezi tangu mwaka 2016 katika jiji la Kigali, sasa, mara mbili kila mwezi watoto na watu wazima kutoka matabaka mbalimbali huendesha baisikeli, hutembea kwa miguu na kufanya mazoezi katika maeneo ya Kigali yaliyotengwa kwa ajili ya sherehe hiyo. Serikali imehakikisha kuwa vipimo vya matibabu na ushauri wa afya unatolewa bure. Hii imepunguza hatari ya magonjwa kama ugonjwa wa moyo na kisukari.

Ijulikane kwamba, si miji yote ya Afrika iliyojiunga na mradi huu. Miji mingine inafanya mambo mengine. Kwa mfano, jiji la Dar es Salaam limetenga barabara maalumu ambapo magari binafsi hayaruhusiwi kuendeshwa. Barabara hizo ni kwa ajili ya mabasi maalumu yanayoitwa mabasi ya mwendo kasi, ambayo huenda haraka na yameweza kupunguza uchafuzi wa mazingira.

Ingawa watu wengi wanapenda wazo la kuwa na maeneo au siku ambapo magari hayatumiwi, mimi nina mawazo tofauti. Ninafikiri bora kuweka faini za magari kuingia mijini siku yoyote. Jambo hili limefanikiwa sana London ambapo kuwepo kwa tozo kuingia katikati ya mji kumedhibiti wingi wa magari katika mji huo wa Ulaya. Kwa hivyo watu hujitahidi kutoendesha ili kuepuka malipo. Ninafikiri



DO NOT WRITE IN THIS MARGIN

https://xtremepape.rs/

serikali za mitaa zingeongeza bei ya malipo ya kuegeshea gari. Kwa namna hiyo, watu wangeacha magari yao nyumbani na kutumia usafiri wa umma. Pia London ina njia maalumu kwa waendesha baisikeli ili kuhakikisha waendeshaji wanasafiri salama.

Nchini Marekani, hakuna usafiri wa umma mwingi katika miji mingi. Kwa hivyo si kawaida kukuta usafiri kama wa mabasi, treni za chini ya ardhi na treni za umeme katika majimbo mengi. Watu wengi huishi mbali na mji na hulazimika kutumia magari binafsi ili kuenda kazini. Miji kama Los Angeles inategemea magari binafsi kwa hivyo sidhani kama tozo lingekubalika kirahisi. Kwa sasa, mji mmoja ambao umejaribu kupunguza foleni za magari ni New York. Inaonekana New York imefuata nyayo za London ingawa tozo huko Marekani ni pungufu kidogo kuliko London.

Andika maelezo mafupi chini ya vichwa vya habari (**17–19**) vinavyotokana na makala uliyoyasoma.

**17** Miji iliyo nje ya Afrika imechukua hatua gani kupunguza utumiaji wa magari mijini:

- ..............................................................................................................................
- ..............................................................................................................................
- ..............................................................................................................................

[3]

**18** Mawazo ya mwandishi kuhusu kutotumia magari mijini:

- ..............................................................................................................................
- ..............................................................................................................................
- ..............................................................................................................................

[3]

**19** Athari za kiuchumi zinazohusu udhibitishaji wa magari

- ..............................................................................................................................
- ..............................................................................................................................
- ..............................................................................................................................

[3]

[Jumla: 9]

Katika **zoezi 4**, utatumia maelezo haya kutunga ufupisho.

DO NOT WRITE IN THIS MARGIN

© Cambridge University Press & Assessment 2026



https://xtremepape.rs/

## Zoezi 4

**20** Sasa tunga ufupisho unaoonyesha faida na hasara za kutotumia magari mijini. Unaweza kutumia maelezo yako mengine kutoka zoezi 3 ili kukusaidia.

Ufupisho wako usizidi **maneno 100**.

Tumia maneno yako mwenyewe kadiri iwezekanavyo.

Utapata alama zisizozidi 4 kwa maudhui ya ufupisho wako, na alama zisizozidi 6 kwa lugha makini na sahihi.

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

[Jumla: 10]

DO NOT WRITE IN THIS MARGIN

© Cambridge University Press & Assessment 2026


https://xtremepape.rs/

## Zoezi 5

**21** Umepata nafasi ya kuwakilisha nchi yako katika michezo ya Olimpiki. Andika blogu itakayosomwa na watu duniani pote. Unapaswa kutaja:

- Mchezo utakaoshiriki
- Jinsi unavyojitayarisha kwa mashindano
- Wasiwasi kuhusu safari

Blogu yako isizidi **maneno 120**.

Utapata alama zisizozidi 3 kwa maudhui ya blogu yako, na alama zisizozidi 5 kwa mtindo na umakini wa matumizi ya lugha yako.

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

[Jumla: 8]

DO NOT WRITE IN THIS MARGIN

© Cambridge University Press & Assessment 2026


https://xtremepape.rs/

## Zoezi 6

**22 ‘Lazima kuenda safari ili kupumzika wakati wa likizo.’**

Je, unakubaliana na wazo hili?

Andika makala katika gazeti la shule ili kutoa maoni yako. Makala yasizidi **maneno 200**.

Safari ni kupoteza pesa. Unaweza kupumzika popote.

Watu hupumzika zaidi wanapokuwa sehemu mpya.

Unaweza kutumia maoni ya hapo juu, na pia ni lazima kutumia mawazo yako mwenyewe.

Utapata alama zisizozidi 8 kwa maudhui ya makala, na alama zisizozidi 8 kwa mtindo na umakini wa matumizi ya lugha yako.

© Cambridge University Press & Assessment 2026



https://xtremepape.rs/

DO NOT WRITE IN THIS MARGIN

DO NOT WRITE IN THIS MARGIN
DO NOT WRITE IN THIS MARGIN
DO NOT WRITE IN THIS MARGIN
DO NOT WRITE IN THIS MARGIN
DO NOT WRITE IN THIS MARGIN

[Jumla: 16]

© Cambridge University Press & Assessment 2026


https://xtremepape.rs/

BLANK PAGE

DO NOT WRITE IN THIS MARGIN
DO NOT WRITE IN THIS MARGIN
DO NOT WRITE IN THIS MARGIN
DO NOT WRITE IN THIS MARGIN
DO NOT WRITE IN THIS MARGIN



https://xtremepape.rs/

BLANK PAGE

DO NOT WRITE IN THIS MARGIN
DO NOT WRITE IN THIS MARGIN
DO NOT WRITE IN THIS MARGIN
DO NOT WRITE IN THIS MARGIN
DO NOT WRITE IN THIS MARGIN



https://xtremepape.rs/

BLANK PAGE

DO NOT WRITE IN THIS MARGIN DO NOT WRITE IN THIS MARGIN DO NOT WRITE IN THIS MARGIN DO NOT WRITE IN THIS MARGIN DO NOT WRITE IN THIS MARGIN

Permission to reproduce items where third-party owned material protected by copyright is included has been sought and cleared where possible. Every reasonable effort has been made by the publisher (Cambridge University Press & Assessment) to trace copyright holders, but if any items requiring clearance have unwittingly been included, the publisher will be pleased to make amends at the earliest possible opportunity.

To avoid the issue of disclosure of answer-related information to candidates, all copyright acknowledgements are reproduced online in our Copyright Acknowledgements Booklet. This is produced for each series of examinations and is freely available to download at www.cambridgeinternational.org after the live examination series.

Cambridge International Education is the name of our awarding body and a part of Cambridge University Press & Assessment, which is a department of the University of Cambridge.

© Cambridge University Press & Assessment 2026



https://xtremepape.rs/